# FAQ

## Maswali yanayoulizwa mara kwa mara

## &

# 2024 Fomu ya Maombi

## Tarehe ya mwisho ya kutuma maombi ni lini?

Applikesheni ya YCJF imefunguliwa hadi tarehe 1 Julai, 2024, 23:59UTCT

## Ninaweza pata wapi fomu ya applikesheni?

Ndio hii kiungo cha mtandao kukuelekeza kwa applikesheni yetu application form , pahali unaweza fanya applikesheni moja kwa moja kwa kubonyeza lugha inayokufaa. Tovuti yetu ya applikesheni- https://youthclimatejusticefund.submittable.com/submit - inapatikana katika Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kihindi, kireno, Kihispania, na kiswahili.

## Je, ninahitaji kuunda akaunti ili kuwasilisha maombi?

Ukitembelea fomu ya maombi na kubofya "submit", utatakiwa kuunda akaunti kwenye mfumo wa Submittable kwa kutumia barua pepe yako binafsi, kisha kuunda nenosiri au nywila na hatimaye kujaza jina lako la kwanza na la mwisho.




Utakapomaliza, utapokea barua pepe kutoka mfumo wa Submittable ikikuomba uthibitishe anwani yako ya barua pepe. Bonyeza kiungo kuthibitisha, na unaweza kuanza kujaza fomu yetu ya maombi.

YCJF

## Nilijiandikisha kwenye mfumo wa Submittable lakini sijapokea barua pepe ya uthibitisho?

Inaweza kuchukua hadi dakika 15 kupokea barua pepe ya uthibitisho. Tafadhali fungua upya kikasha chako cha barua pepe na uangalie vikasha vyote (ikiwa ni pamoja na spam/junk, updates, nk) ili kuhakikisha hupitwi na barua pepe hiyo.

## Je, ninaweza kuhifadhi maombi yangu na kuendelea baadaye?

Ndiyo. Unaweza kuhifadhi majibu yako na kurudia fomu ya maombi yako baadaye. Kumbuka kubofya kuhifadhi wakati unajibu swali jipya. Ikiwa simu au kompyuta yako inaishiwa umeme, kifurushi cha mtandao au unahitaji kusitisha kujaza fomu ili kushughulikia jambo la dharura, bofya tu kuhifadhi na utapokea kiungo kwenye barua pepe yako ambacho unaweza kutumia kuendelea na maombi yako baadaye. Zingatia tahadhari hii: Bofya kitufe cha "submit" punde tu baada ya kumaliza fomu yote.

## Je, inachukua muda gani kujaza fomu ya maombi?

Inachukua takribani kati ya dakika 30 hadi 60 kukamilisha maombi yako.

## Je, ninaweza kuwasilisha maombi yangu kupitia barua pepe?

Njia pendekezwa ya kuwasilisha maombi ni kupitia tovuti yetu ya maombi mtandaoni ambayo unaweza kulipata hapa: https://youthclimatejusticefund.submittable.com/submit . Katika hali ambapo waombaji hawawezi kufikia jukwaa la maombi mtandaoni, wanaweza kuwasiliana na Viongozi wetu wa Kanda kupitia barua pepe ask@ycjf.org ili kufanya kazi nao kupata suluhisho la kuwasilisha maombi yao.

## Nani anaweza kuomba kwenye Youth Climate Justice Fund?

Vikundi vinavyoongozwa na vijana ambavyo ni jumuishi, vina mtazamo wa kijumuisha na vinavyopigania juhudi za pamoja kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Tafadhali soma vigezo vyetu hapa: https://ycjf.org/howto-apply

## Je, ninahitaji kuwa nimesajiliwa kisheria?

Hapana, usajili wa kisheria au rasmi hauhitajiki.

## Je, mtu binafsi anaweza kuomba mfuko?

Lengo letu ni kufadhili harakati na waandaaji kutoka kwenye nyanja za msingi katika jamii. Hii inamaanisha mtu binafsi anaweza kuomba ikiwa kazi yake ni sehemu ya/inaunga mkono kikundi kilichotambuliwa au kikundi cha haki za hali ya hewa.

## Tumeanzisha shirika au kikundi chetu hivi karibuni, je, bado tunaweza kuomba kwani tuko wapya?

Ndiyo! Kila shirika linaloongozwa na vijana au kikundi wanaweza kuomba bila kujali kama kimeanzishwa hivi karibuni au kina uzoefu wa miaka kadhaa.

## Je, ninaweza kuwasilisha maombi zaidi ya moja?

Hapana. Kutokana na idadi kubwa ya maombi, tunapendekeza waombaji kuwasilisha ombi moja kwa kila kikundi, shirika au mtu binafsi. Unaweza kuelezea miradi yako kwenye fomu ya maombi.

## Kikundi changu hakina bajeti ya kila mwaka. Tunapaswa kufanya nini?

Bajeti ya kila mwaka si hitaji. Ikiwa ni kikundi kipya kilichoanzishwa bila bajeti ya kila mwaka, chagua 'hapana' wakati unajibu swali hilo.

## Bajeti yangu ya kila mwaka ni zaidi ya $100,000. Je, mimi si stahili?

Wito wetu wa sasa wa mapendekezo ni kwa vikundi vinavyoanza ambavyo havina rasilimali. Vikundi hivi vinaweza kuomba hadi $20,000 kusaidia kazi zao za msingi au shughuli za mradi. Vikundi vilivyoimarika vizuri na bajeti ya kila mwaka ya zaidi ya $100,000 havistahili kwa wito wa maombi wa sasa. Badala yake, unaweza kuwasiliana nasi kujadili ushirikiano wa uwezekano.

## Ninawezaje kupakua na kupakia bajeti kwa kutumia kiolezo/ mfano/ mwongozo uliotolewa?

Unaweza kupakia bajeti yako katika muundo unaopendelea. Pia tumetoa kiolezo cha bajeti katika fomu ya maombi kwenye Submittable ambacho unaweza kutumia. Pakua kiolezo, ujaze, na upakie katika sehemu ya bajeti ya fomu ya maombi ya mtandaoni.

YCJF

## Siwezi kupata kanda yangu kwenye orodha, nifanye nini?

Hatuko kamili katika mgawanyo wa kanda. Tunakuhimiza uombe ukitumia kanda iliyo karibu na yako. Kwa mfano, ikiwa unatoka Western Balkans, unaweza kuchagua Ulaya na Asia ya Kati.

### Ninaweza kutarajia lini kujua matokeo ya maombi yangu?

Tutakuwa tukitathmini na kuhakiki maombi kadri yanavyokuja kwa sababu tunapokea idadi kubwa ya maombi. Tunatarajia kuarifu waombaji wote kuhusu uamuzi wetu ifikapo Septemba 30, 2024.

## Ikiwa mradi wangu utachaguliwa, nitapokea lini fedha?

Uhamisho wa ruzuku unatarajiwa kufikia waombaji wote waliofanikiwa ifikapo Desemba 31, 2024. Hii inamaanisha unapaswa kupanga kutekeleza mradi wako mwaka 2025.

## Nataka kushirikiana na YCJF kusaidia mradi wangu

Wapokeaji wetu wa ruzuku ni washirika wetu. Hatua ya kwanza ya ushirikiano ni kuomba ruzuku yetu. Tafadhali wasilisha maombi kwenye jukwaa letu na eleza mahitaji yako ya ushirikiano chini ya maelezo ya mradi.

## Siwezi kupata Kiongozi wa Kanda kwa kanda yangu kwenye tovuti yako, nifanye nini?

Viongozi wetu wa Maeneo bado wanasafirishwa kwa hivyo endelea kuangalia tovuti yetu kwa habari mpya. Kwa sasa tuna viongozi 5 wa maeneo wanaojumuisha Asia Kusini, Asia-Pasifiki, Afrika Kusini, Jangwa la Sahara, Amerika ya Kusini na Karibea, na Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini. Viongozi wa Maeneo si lazima wawe wawakilishi wa eneo zima bali ni watu binafsi ambao wanaweza kufanya kazi ili kusaidia washirika wetu wanaopokea hazina katika eneo hili. Wasiliana na viongozi wetu wowote wa eneo ikiwa huna uhakika wa eneo unaloishi na watakusaidia.

## Sihitaji ufadhili. Je, naweza kuomba msaada wa kujengewa uwezo?

IIkiwa huna haja ya ufadhili lakini una nia ya mpango wetu wa kujenga uwezo, tuma barua pepe kwa hello@ycjf.org na maelezo kuhusu aina ya uwezo unaotaka.

# Maswali yanayoulizwa mara kwa mara kuhusu YCJF

## Je, tunamaanisha nini kwa 'kushughulikia hali ya hewa na haki ya kijamii na kimazingira'?

Tunamaanisha masuluhisho, kampeni, na miradi inayoshughulikia mzozo wa hali ya hewa kwa kushughulikia kwa upamoja ubaguzi, unyonyaji, na ukandamizaji, na kuimarisha nguvu ya jamii, usawa na haki.

## Tunamaanisha nini kwa 'kuongozwa na vijana'?

Tunaamini kwamba "vijana" hushikilia maana nyingi na miktadha kutegemea mitazamo na miktadha ya ulimwengu. Tunaamini kwamba usawa kati ya vijana walio chini ya umri wa miaka 35 ambao wanabaguliwa au kutengwa kwa misingi ya tabaka, kabila, utambulisho wa Watu wa Asili, jinsia, n.k. na wanaharakati wachanga sana ambao pia wanakabiliwa na changamoto sawa , ni muhimu.

## Je, mpango wa uwezo wa "vijana-kwa-vijana" ni nini?

Vijana wanaosaidiana katika kukuza uwezo wa rika kwa rika ndio watoa huduma bora wa maendeleo kutokana na uzoefu na kuelewa kwao wa pamoja. Tutashirikiana kujenga na kuboresha ukuzaji wa uwezo wa vijana-kwa-vijana kulingana na kila kundi la washirika wanaopokea hazina.

## Je, YCJF inafadhiliwa vipi?

Gharama zetu za awali za kuanza na ufadhili wa mbegu hutolewa na watu binafsi na wahisani - badala ya kampuni za kibinafsi au zilizoorodheshwa. Hatukubali ufadhili kutoka kwa mtu yeyote ambaye haendani na kanuni na maadili yetu.

## Tunaweza kuomba hadi $20000 USD, lakini je, tunaweza kutuma applikesheni hata kama jumuiya yetu inahitaji hazina zaidi?

Katika hatua hii, vikundi vya ndani na kitaifa vinaweza kutuma applikesheni ya hadi $20000 pekee.

YCJF

## Sisi ni kikundi kinacholenga kikanda au kimataifa. Je, tunaweza kutuma applikesheni?

Wito wetu wa wazi wa 2024 ni wa vikundi vya kitaifa na vya mtaa pekee.

*Tafadhali soma kwa makini na ututumie barua pepe tu ikiwa maswali yako hayajajibiwa. Tafadhali kumbuka kuwa hatutajibu barua pepe na maswali ambayo tayari yamejibiwa hapa au kwenye tovuti yetu.

# 2024 Fomu ya Applikesheni

*Tafadhali kagua maswali ya Applikesheni la 2024 kabla ya kuwasilisha kupitia Submittable.

## SECTION A - VIGEZO VYA KUSTAHIKI

### Je, kikundi chako ni shirika/kikundi kinachoongozwa na vijana?

Ndio / Hapana*

*Tafadhali kumbuka kwamba ikiwa shirika/mkusanyiko wako hauongozwi na vijana, hustahiki kutuma applikesheni yetu ya hazina.

## Je, kikundi chako kimesajiliwa kisheria na akaunti rasmi ya benki ili kupokea hazina? (Tafadhali kumbuka kuwa vikundi vilivyosajiliwa na visivyosajiliwa vinastahiki kutuma ombi kwa YCJF)

Ndio / Hapana

## Ikiwa sivyo, je, una mfadhili wa kifedha au shirika ambalo linaweza kupokea hazina kwa niaba yako ikifaulu?

## Kundi lako liko katika eneo gani?

(Wanaotuma applijesheni kutoka nchi zilizo na mapato ya juu wanapaswa kuwa wa kikundi cha wachache au vikundi visivyo na uwezo wa kuzingatiwa ili kupata ufadhili. Vikundi vinavyoangazia shughuli za kimataifa bila kazi yoyote ya kijamii haviruhusiwi kutuma applikesheni)

- Asia ya Mashariki na Pasifiki
- Ulaya na Asia ya Kati
- Amerika ya Kusini na Karibiani
- Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini
- Marekani Kaskazini
- Asia ya Kusini
- Afrika Jangwa la Sahara

*Tafadhali zingatia ramani iliyo hapa chini ili kutambua eneo lako




YCJF

## Je, uongozi wa kikundi chako unajihusisha na mojawapo ya yafuatayo:

- Wanaoongozwa na wenyeji
- Inayoongozwa na Womxn (ikiwa ni pamoja na uongozi wa wanawake, uongozi usio wa binary, nk).
- LGBTQI2S+ -led
- Inaongozwa na jamii ya ndani
- Wanaoongozwa na watu wa rangi
- Wale wenye uwezo tofauti
- Wakimbizi wanaoongozwa
- Wanaoongozwa na watoto

## Je, watu walio katika nafasi ya kufanya maamuzi ya kikundi chako wana umri gani?

- 19 na chini
- 20 - 24
- 25-29
- 30 - 35
- 35 na juu

## Je, angalau 75% ya jumuiya inayohudumiwa na kikundi chako iko chini ya umri wa miaka 35?

Ndio / Hapana

## Je, kazi ya kikundi chako inalenga kuwawajibisha watunga sera?

*Hii inaweza kujumuisha (lakini haizuiliwi) kampeni na shughuli zinazolenga kuwahimiza au kusaidia watoa maamuzi kutekeleza ahadi zao za hali ya hewa na mazingira.

Ndio/Hapana

## Je, kazi ya kikundi chako inalenga katika kuinua tamaa ya hatua za usawa na haki za hali ya hewa?

*Hii inaweza kujumuisha (lakini haizuiliwi) shughuli zinazolenga swala la kukosekana kwa dharura kwa hali ya hewa na hatua za kimazingira kwa kuwasilisha masuluhisho ya kiasili yanayoongozwa na wenyeji, na mbinu ambazo zinaweza kuongezwa na serikali, biashara na jamii.

Ndio\Hapana

## Je, kazi ya kikundi chako inalenga katika kukuza uongozi mbalimbali unaojikita katika utendaji wa haki na usawa wa hali ya hewa?

*Hii inaweza kujumuisha (lakini haijazuiliwa) shughuli zinazojenga uongozi wa vijana kwa njia za vitendo ili kuongeza nguvu ya jumuiya na ya pamoja katika kupiga hatua za hali ya hewa.

Ndio/ Hapana

## Je, kikundi chako kina bajeti ya kila mwaka?

Ndio/Hapana

## Kama ndiyo, bajeti ya mwaka ni kiasi gani?

(Wito wa wazi wa YCJF hutanguliza makundi yanayoibukia. Tunatambua kwamba vikundi vilivyoanzishwa na vinavyoongozwa na vijana vilivyo na bajeti ya kila mwaka ya zaidi ya $100,000 vinaweza kukabili changamoto kuendeleza kazi zao. Ikiwa uko katika kitengo hiki na unaamini kuwa kazi yako inalingana nasi, tafadhali wasiliana nasi kupitia ask@ycjf.org)

- 0 - 10,000
- 10-25,000
- 25-50,000
- 50,000 - 100,000
- 100,000 na juu

*Kiwango cha bajeti katika USD

## SECTION B - MAELEZO YA KIKUNDI/MRADI

Ikiwa umefikia hatua hii, inamaanisha kuwa umestahiki kufanya applikesheni. Ikiwa unahitaji usaidizi wowote wa kukamilisha applikesheni yako tafadhali wasiliana na Viongozi wetu wa Maeneo kupitia ask@ycjf.org

### Jina la kikundi chako

Jibu fupi

### Eneo la msingi la kazi ya kikundi chako ni lipi?

Jibu fupi (orodha ya maeneo)

### Jina la Kiongozi wa Pendekezo

*Mtu anayefanya appilkesheni

Jibu fupi

### Nafasi ya Kiongozi wa Pendekezo katika kikundi

Jibu fupi

### Tarehe ya Kuzaliwa ya Kiongozi wa Pendekezo

DD/MM/YYYY

### Jinsi ya mawasiliano ya kikundi (barua pepe/whatsapp, telegraph, ishara/simu)

Jibu fupi

## Nini lengo la msingi na dira ya kimkakati ya kikundi chako?

Jibu fupi

## Eleza kwa ufupi mradi/shughuli kuu ambayo kikundi kinatafuta usaidizi.

Jibu fupi
*Maneno yasizidi 200 – (Hii inaweza kuwa kitu chochote kutoka kwa shughuli maalum za kikundi chako au kudumisha tu wafanyikazi wako na gharama za uendeshaji).

## Je, timu imefaulu katika nini hadi sasa na hazina hii itaendeleza vipi juu ya mafanikio yako yaliyopo, ikiwa yapo?

Jibu fupi
*Eleza kwa ufupi tatizo ulilopata na ukalishughulikia hapo awali ambalo linaweza kuwa linahusiana au halihusiani, na jinsi uzoefu huo unavyoweza kuongezwa kupitia hazina hii.

## Je, mafanikio yako ya awali na mradi wa sasa unalingana na malengo ya YCJF ya kuwawajibisha watunga sera, kuinua ari ya usawa na haki juu ya hali ya hewa na hatua za kimazingira, na kukuza uongozi wa vijana unaojikita katika nguvu ya jamii?

Jibu fupi
*Maneno yasiyozidi 100

## Orodhesha washirika wowote ambao kikundi chako kinafanya kazi nao.

Jibu fupi
*Maneno yasiyozidi 50

## Je, ni kwa jinsi gani kikundi chako kinajumuisha au kupanga kujumuisha kanuni za haki, utofauti, na ushirikishaji katika juhudi zinazolenga kusaidia makundi ambayo hayajahudumiwa?

Jibu fupi
*Maneno yasiyizidi 100

## Unakiona wapi kikundi chako miaka 3 kutoka sasa?

Jibu fupi
*Maneno yasiyizidi 100

## Je, unaomba kiasi gani cha ufadhili? (vikundi vya mashinani vinaweza kutuma maombi kutoka $10,000 hadi $20,000. Makundi ya kimataifa na ya kikanda yenye mahitaji makubwa ya ufadhili yanaweza kuwasiliana nasi kupitia ask@ycjf.org. Vikundi kama hivyo vinaweza kutuma maombi ya hadi $50,000)

Jibu fupi

## Utatumia pesa katika namna gani? Tafadhali weka bajeti yako

Unaweza kupakua templeti ya bajeti kutoka here

## Je, ni mahitaji gani ya kujenga uwezo na maendeleo ya shirika ambayo kikundi chako kinahitaji pamoja na ufadhili?

*Tunawezaje kukusaidia zaidi ya hazina hii

Jibu fupi

YCJF

Ili kutusaidia kuelewa vyema kikundi chako na kazi unayofanya, tafadhali toa hati, viungo, au faili zozote zinazofaa kama vile ripoti za mradi, ripoti za kila mwaka, machapisho, madokezo ya simulizi au rekodi za sauti/video za shughuli za hivi majuzi.

Ninakubaliana na sera ya YCJF ya kutunza taarifa zilizotolewa katika maombi haya kwa mzunguko wa ruzuku wa YCJF 2024.

☐

YCJF